

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

Simu Na: +255 (026) 2740016  
Nukushi: +255 026 2740103  
Barua Pepe: [ded@makededc.go.tz](mailto:ded@makededc.go.tz)



Tovuti: <http://www.makededc.go.tz>

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,  
S. L. P 6,  
**MAKETE.**

***Unapojibu tafadhali taja;***

**Kumb. Na. EA.172/302/01/145**

**29 Septemba, 2021**

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA  
AJIRA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia nafasi moja ya kazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

**1. SIFA ZINAZOHITAJIKA**

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe na taaluma inayohusu Utawala na Rasilimali watu au Sheria
- iv. Awe mkazi wa eneo la kiutawala la Halmashauri ya wilaya ya Makete
- v. Asiwe Mtumishi wa umma (awe mstaafu)
- vi. Awe na umri kuanzia miaka 55 na kuendelea
- vii. Asiwe na makosa ya jinai au kuachishwa kazi kwa makosa ya Jinai.

## 2. MALIPO

- Kazi hii haina malipo ya mshahara isipokuwa inakuwa na malipo ya posho pindi kunapokuwa na kikao.

## 3. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

- Kuongoza vikao vyote vya bodi vinavyohusu
  - ✓ Ajira mpya kwa watumishi
  - ✓ Kuthibitisha watumishi kazini
  - ✓ Upandishaji wa vyeo kwa watumishi
  - ✓ Kubadilisha kazi watumishi kulingana na miundo ya utumishi wa umma.

**NB:** Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji ((W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,  
S.L.P. 6,  
MAKETE.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **13/10/2021** saa **9:30 alasiri** na wale watakaokuwa wamekidhi vigezo na kuteuliwa katika mchujo wa awali wataarifiwa.



Humphrey A. Mushi  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**Halmashauri ya Wilaya ya Makete**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
MAKETE**